


SURA YA 4

KUTOKA



WALITEMBEA HADI KUFIKA MILIMANI
KANDO YA BAHARI YA SHAMU. WALIPIGA
KAMBI HUKO WAKIZUNGUMZA JINSI
WANGWEZA KUVUKA BAHARI SHAMU.



BAADA YA FARAO
KUOMBOLEZA
MWANAWA
ALIJAWA NA
HASIRA ZAIDI.

**TAYARISHENI
MSAFARA! MUWAFUATE
WAEBRANIA. MUWARUDISHE
HUKU AMA MUWALIE.**

TUTAFANYA
UTAKAVYO,
MKLIBWA.



**TAZAMA, JESHI
LA MISRI LINAKUJA!
TUMEFUNGIWA
JANGWANI.**

**MUSA ALITULETA HAPA
TUFE. INGEKUWA VYEMA
TUBAKI WATUMWA KULIKO
KUFIA HUKU.**



HAKUNA
LOLOTE MUNGU
ANAZEWA FANYA
KUTUOKOA SASA.



MILIMA IKO MBELE
YETU NA BAHARI PIA.
TUMETEGWA.

WAMISRI WALIPOWAONA WAEBRANIA
NA WALIPOKUMBUKA JINSI
MUSA ALIFANYA MISRI ITESEKE,
WALIKUWA TAYARI KUWALIA.



SIMAMENI MLIKO.
MUNGU ATATUOKOA KWA
NJIA KUU.

MUNGU AMELIKAUSA MOYO
WA FARAO TENA. BAADA YA LEO
HAMTAWAHI KULIONA JESHI LA
MISRI TENA.

KUTOKA 14:5-13



JESHI LA MISRI LILIPOKUWA KARIBU KUFIKIA
WAEBRANIA, MOTO MKUBWA ULITOKA MBINGUNI NA
KUFUNGA NJIA. USIKU HUU, WAEBRANIA WALIONA
MWANGAZA ILHALI WA MISRI WALILIONA GIZA TUPLI.

MUSA ALIINUA FIMBO YAKE JUU NA UPEPO MKUBWA ULIKUJA TOKA MBINGUNI, UKAGAWANYA MAJI NA KUKAWA NA NJIA KATI YA BAHARI.



HUU ULIKUWA MUJIZA MKUBWA SANA. WANA WA ISRAELI WALITEMBEA KATI YA BAHARI KWA NCHI KAVU.

SIKU ZILIZOKUJA WALIIMBA KUHUSU MUNGU ALIYEFANYA NJIA KATIKATI YA BAHARI. KILA MTU ALIFAHAMU KUWA KUNA MUNGU MMOJA TU NA JINA LAKE NI YEHOVA.



HII IMEPITA KILA
KITU TULICHOKIONA
MISRI.


KWELI MUNGU WETU NI
MWEMA KULIKO WOTE.



**JOSAYA! LINA
WAZIMU? ONDOKA
HAPO. LINAJUA HUWEZI
KUOGELEA.**



NATAKA
KUWAGUZA SAMAKI
HAWA WANAOPENDEZA.



WAEBRANIA WALIPOKUWA KARIBU
KUVLIKA, MUNGU ALIONDOA MOTO
ULIOKUWA LIMEPINGA WAMISRI.
HAWAKUWA WAMEONA BAHARI
IKIWA IMEJIGAWANYA, KWA HIVYO
WAKAKIMBIA KUWAFIKIA WAEBRANIA.


**MBELE,
WAUENI
WAEBRANIA!**

KUTOKA 14:22-23




LEO MUMEONA UWEZO WA
YEHOVA.

TAZAMA, MAJI YANARUDI.
WATAZAMA.



KILA MWANAJESHI WA MISRI AZLIZAMA
KWENYE BAHARI. MILINGU YAO YA
MBAO NA MAWE HAINGEWASAIDIA.

KUTOKA 14:27-28




TAZAMA
MIILI HII YOTE.
BAHARI IMEJAA
WANAJESHI WA
MISRI WALIOKUFA.

KWA KWELI
YEHOVA NDIYE
BWANA MUNGU PEKEE.
HAKUNA MUNGU MWINGINE
AWEZAYE KUTENDA HAYA.
TUTAIKUMBUKA SIKU HII
MILELE NA MILELE.

WALIPOACHA BAHARI NA JESHI LILILOKUFA LA MISRI, WATOTO WA KIEBRANIA WALIMFUATA MUSA NA LILE WINGU NYIKANI. WALIENDELEA KULA NA KUNYWA CHAKULA WALICHOTOKA NACHO MISRI.




BAADA YA SAFARI YA SIKU CHACHE, WINGU LILILOKUWA LIKIWAONGOZA LILISIMAMA KARIBU NA KISIMA CHA MAJI. WAEBRANIA WALIPIGA KAMBI HAPO HADI CHAKULA CHAO KIKAKWISHA. HAWAKUWA NA MAHALA PENGINE PA KUPATA CHAKULA. HAPAKUWA NA MATUMAINI.



TUNGEBAKI MISRI NA TUNGEISHI
VYEMA KULIKO HIVI. TULIPOKUWA
WATUMWA TULIKUWA NA CHAKULA CHA
KUTOSHA. HAPA HAMNA CHOCHOTE.

NDIO. ULITULETA
HAPA TUFE KWA NJAA?



NISIKILIZENI,
HAMNILALAMIKII MIMI
BALI MNAMLALAMIKIA
MUNGU
TUNAYEMFUATA.

YHOVA ASEMA ATASHUSHA
MKATE KUTOKA MBINGUNI. KILA
ASUBUHI MTAPATA MKATE ARDHINI.
MTAKACHOFANYA NI KUOKOTA NA
KULA.



MUSA
AMESEMAJEE?
TUTAPATAJE CHAKULA?
WATOTO WETU
WANATESEKA.

ANASEMA KUWA
YEHOVA ATASHUISHA MKATE
KUTOKA MBINGUNI KILA
ASUBUHI.



NI WAKATI JUA LIPAE SASA. UNAAMINI
KUTAKUWA NA MKATE ARDHINI KAMA
MUSA ALIVYOSEMA?

TUTATESEKA
KWA NJAA
TUKIKOSA
MKATE.

USHAWHI
KUSIKIA MKATE
UKIANGUKA KUTOKA
MBINGUNI?


LA, ILA SIJAWAHI
KUSIKIA KUHUSU
NJIA KUFANYIKA
KATIKATI YA BAHARI.
MUNGU HUYU WA
MUSA LAZIMA
AWE MUUMBAJI
WA ULIMWENGU.
SIDHANI NI NGUMU
KWAKE KUSHUSA
MKATE KUTOKA
MBINGUNI. NJOO,
NI WAKATI TWENDE
TUKAANGALIE.

KUTOKA 14:21-22, 30, 16:2-3, 7-8



MKATE
ULIOTOKA
MBINGUNI. KAMA
ALIVYOSEMA.

MBONA
SISI HUWA
NA SHAKA?



**TAZAMA! IKO
KILA MAHALI.**

**AH, NI TAMU.
INAONJA KAMA
ASALI.**

**KWA KWELI YEHOVA NI
MUNGU NA MUSA NI NABII
WAKE.**

WALIPOKUWA NYIKANI MUNGU
ALIWALISHA CHAKULA KILA SIKU NA
CHAKULA CHA MALAIKA CHA MBINGUNI.




WINGU LILIPOKUWA JUU YA KAMBI WALIENDELEA KUKAA
KANDO YA KISIMA CHA MAJI NA KULA MKATE ULE,
LAKINI PINDI WINGU LILIPOANZA KUONDOKA WALIPANGA
VIRAGO VYA NA KUANZA KUSAFIRI WAKILIFUTA NYIKANI.

ILA ILIFIKA WAKATI AMBAPO
MAJI YALIWAISHIA.

KWA HIYO
ALITUPATIA MKATE
NA SASA ANATAKA
KUTULUA KWA KIU?

MSICHANA
WANGU MDOGO
ATAAGA ASIPOPATA
MAJI YA KUNYWA.





TUNGEBAKI TU MISRI.
KWA SIKU NYINGINE MIFUGO YETU
YOTE ITAKUFA NA BAADAYE WATOTO WETU
PIA WATAANZA KUFA. TUNAFAA KUGONGA
VICHWA VYETU NA MAWE.

MUNGU
YUPO NA
SISI AU LA?

NITAKWENDA
NIZUNGUMZE NA
YEHOVA.

KUTOKA 16:14-15, 17:2-4, ZABURI
78:24-25



MUNGU ALIMWELEZA
MUSA CHA KUFANYA.

NJOONI
MUONE LIWEZO WA
YEHOVA. HAMULIAMINI,
MNALALAMIKA TU.

ALIWAPATIA MKATE,
NA SASA ANAWAPATIA MAJI
KUTOKA KWA JIWE HILI.



WHAAACK!

IEEE!

MAJI YALITIRIRIKA
KAMA YA MTO.






TENA WINGU LILISONGA NA WAEBRANIA
WAKAPANGA VIRAGO NA KUANZA SAFARI
WAKILIFUATA WINGU NYIKANI KULEKEA
KWA MLIMA ULIOULIKANA KAMA SINAI.

HUKO MUSA ALISALI NA MUNGU
ALIZUNGUMZA NA YEYE.

**WAKUMBUSHE YALE
YOTE NILIYOWAFANYIA WANA
WA MISRI, NILIVYOWAOKOA,
NIKAWALISHA NA KUWANYWESHA
KUTOKA KWA JIWE.**






**WAELEZE
IWAPO WATATII
AMRI ZANGU
NIATAWAFANYA
WATU WANGU WA
KIPEKEE DUNIANI
KOTE. WAKITII AMRI
ZANGU NITAWAFANYA
UFALME WA
MAKUHANI.**

**MUSA,
NIKIZUNGUMZA
NANYI NITAKUJA
KAMA WINGU NONO
ILI WATU WAWEZE
KUONA NA KUSIKIA
KWAMBA NI MIMI.**

MUSA ALITOKA JUU MLIMANI NA AKAWAELEZA
WATU YOTE MUNGU ALIYOYASEMA.



TUTATII KILA KITU
AMBACHO MUNGU
ATASEMA.



BASI NENDENI MKAOGA NA KUFUA
NGUO ZENU. MJITAYARISHE KUMUABUDU
MUNGU. SIKU TATU KUTOKA LEO MUNGU
ATAWATEMBELEA.

KAMA MUNGU ALIVYOAMRUI, BAADA YA SIKU
TATU WATU WALIKUSANYIKA MLIMANI WAKINGOJA
MUNGU AWAZUNGUMZIE. WINGU LISILOKUA LA
KAWAIDA LILITUA JULU YA MLIMA ALAFU....



*MUSA, NJOO JULU
MLIMANI.*



**MUSA, MIMI NDIYE YEHOVA
MUNGU, NILIYEWATOA MISRI. UKIRUDI,
WEKA UA KILA MAHALI KUZINGIRA
MLIMA HUU.**

**IWAPO MTU MWINGINE
YEYOTE AKIUSHIKA MLIMA HUU
ATAKUPA AMRI
KUMI AMBAZO LAZIMA
UWAELEZEE WATU.**



MSIWE NA MIUNGU
MINGINE,

MSITENGENEZE SANAMU,

MSILITAJE JINA LA MUNGU
OVYO,


MUIFANYE TAKATIFU SIKU YA
SABATO,

HESHIMU MAMA NA BABA
YAKO.

MSIUE, MSIZINI, MSIIBE,

MSIPEANE USHUHUDA WA
LONGO DHIDI YA MAJIRANI
WENU,

MSITAMANI VITU VYA
MAJIRANI WENU.



MUSA ALIPOSHUKA KUTOKA
MLIMANI ALIWAKUSANYA VIONGOZI
SABINI WA ISRAELI NA KUWAELEZA
KUHUSU AMRI ZA MUNGU.


TUTAFANYA
HIVYO.

NI AMRI NZURI.

NYINYI WATU SABINI MTARUDI
MLIMANI NA MIMI. MTAPATANA NA
MUNGU NA MTAJIONEA WENYEWI. LAKINI
KWANZA LAZIMA NIANDIKE KWA KITABU AMRI
AMBAZO MUNGU ALINIELEZA.

MUSA ALIKUWA MAKINI KUANDIKA
AMRI AMBAZO MUNGU ALIMUELEZA.
ROHO MTAKATIFU ALIMUONGOZA
ASIFANYE MAKOSA YOYOTE.



A comic-style illustration of Moses, with a long beard and wearing a yellow and black robe, standing on the left and reading from a large scroll. He is addressing a large crowd of Israelites on the right, who are dressed in simple, earth-toned clothing. The background shows a hazy, mountainous landscape under a bright sky. The text is presented in three separate boxes: a top box with the title, a middle speech bubble, and a bottom box with the main body of text.

MUSA ALIPOMALIZA
KUANDIKA
ALIWAKUSANYA WATU
ILI KUWASOMEA
MANENO YALE.

YOTE AMBAYO
MUNGU AMESEMA NI
MEMA. NA TUYAFUATA.

KWA HIVYO TAIFA LA ISRAELI
LILIFANYA AGANO NA MUNGU.
ANGWABARIKI, AWAPATIE UHAI NA
KLIWAOKOA KUTOKA KWA MAADUI
WAO. WANGEFUATA AMRI ZOTE ZA
MUNGU NA KUTEMBEA KWA WEMA.

MUNGU ALIMUAMURU MUSA ATOE DHABIHU
YA DAMU NA AWANYUNYUZIE WATU DAMU.



WOTE WALIKUWA WATENDA DHAMBI, WALIFAA KIFO
HATA MUSA NA HARUNI. ILA MUNGU ALIKUWA
NA HURUMA. ALIWAPA NJIA YA KUTOROKEA.



KWA KUNYUNYUZIA DAMU YA MWANA KONDOO, MUNGU ANGEWASAMEHE DHAMBI ZAO NA HANGEWALA KAMA WALIVYOFAA. MWANAKONDOO AMBAYE HANGEFAA KIFO ALIKUFA KWA AJILI YA WENGI WALIOSTAHILI KUFA KWA AJILI YA DHAMBI ZAO.



SASA KWA SABABU DHAMBI ZENU ZIMEFUNIKWA, NYINYI SABINI MTAENDA NAMI MLIMANI NA MTaweza KUONA UTUKUFU WA MUNGU.

KUTOKA 24:1-8



KWA HIVYO VIONGOZI SABINI
WALIKWENDA NA MUSA JULU YA MLIMA
AMBAKO MLINGU ALIZUNGUMZA NA MUSA.

GHAFLA, KITI CHA ENZI CHA
MUNGU KILITOKEA MBELE YAO.



**LITUKUFU
WA MUNGU!**

VIONGOZI SABINI WALIMTAZAMA MUSA
AKIENDA JUU YA MLIMA NA KUPOTELEA
KATIKA UTUKUFU ULIONG'AA WA MUNGU.

INAPENDEZA
SANA!

NA UTUKUFU.


HAKUNA MTU
KAMA MUSA ANAYEWEZA
KUZUNGUMZA NA MUNGU
MOJA KWA MOJA.

KUTOKA 24:9-10

**MUSA, UTAWAELEZA WATU
WAJENGE HEKALU AMBALO
WATAKUWA WAKINIABUDIA.
LITAKUWA NA MADHABAHU AMBAKO
MTATOLEA SADAKA. NA MAHALI
PATAKATIFU AMBAKO NAWENZA
KUKUTANA NA KUHANI MKUU MARA
MOJA KWA MWAKA KATIKA VIZAZI
VYAO VYOTE.**

**NITAKUELEZA JINSI
LILATAKAVYOJENGWA. KABILA
LA LEVI WATAKUWA MAKUHANI
WANGU. HARUNI, PAMOJA NA
WANAWE WATAKUWA MAKUHANI
WANGU. WATAWAFUNZA WATU KUWA
WATAKATIFU NA WATAWATOLEA WATU
SADAKA WATAKAPOTENDA
DHAMBI.**





IMEKUWA NI WIKI
KADHAA TANGU APOTELEE KATIKA
MWANGAZA HUO. LAZIMA AWE
AMEKUFA.

NDIO.
HATUWEZI KUISHI
NYIKANI MILELE.


TUNAHITAJI
MUNGU WA
KUTUONGOZA
KAMA MUSA
ALIVYOFANYA.

TUTENGENEZENI
PICHA YA MUNGU WA
DHAHABU.



MUSA
AMEKUFA. HARUNI
ATATUT **ENG**ENEZEA
MUNGU WA DHAHABU
AMBAYE ATATURUDISHA
MISRI.

TUPATIENI
DHAHABU YENU.




KWA KUTUMIA MIKONO YAO WAJINGA
WALE WALITENGENEZA FAHALI WA
DHAHABU NA KUIITA MUNGU. SURA
YA SHETANI KABLA YAKE KUTENDA
DHAMBI ILIKUWA NI FAHALI, ILA
WATU HAWAKULIJUA HILO.

HARUNI ALIFUATA KAMA WATU WALIVYOTAKA
NA KUWASAIDIA KUJENGA FAHALI YULE.


KUTOKA 20:4, 25:8-9, 28:1-3, 32:1-4, EEKIELI 1:10, 10:14, 28:14

HARUNI ALIKUWA MPUMBAVU SANA.
ALIJUA KUWA FAHALI HAIKUA MUNGU
LAKINI ALIOGOPA KUWAAMBIA WATU.



NDIYE HUYU
MUNGU WENU
ALIEWATOA MISRI. KESHO
NITAOA SADAKA KUBWA ILI
KUMFANYA YEYE KUWA
YEHOVA.

MUNGU ALIKUWA AMEWAAMLIRU
WASIZIABUDU MIUNGU MINGINE ILA
WALIAMUA KUFUATA FIKIRA ZAO.



WATU WALICHEZA NA
KUWA UCHI. WALILEWA
NA KUTENDA DHAMBI
NYINGI. MUNGU ALIKUWA
TAYARI KUWAANGAMIZA NA
KUWATUPA KWENYE MOTO
ULIOTAYARISHIWA SHETANI
NA MALAIKA WAKE.

MUNGU ALIZUNGUMZA NA MUSA NA KUMWAMBIA,
"NENDA CHINI SASA. WATU WAMETENDA DHAMBI
KUBWA. WAMEJIFANYA UCHI NA KUCHEZA MBELE
YA SANAMU. INAFAA NIWAANGAMIZE. MIOYO
YAO NI MIGUMU HAWATEMBEI KWA HAKI."




MUSA ALIKASIRIKA ALIPOONA KWAMBA WATU
WALITENGENEZA SANAMU NA KUMSAHAU MUNGU.

**MUMEVUNJA AMRI
ZA MUNGU.**




MUSA ALIVUNJA JIWE
ALILOKUWA AMEANDIKIA
AMRI ZA MUNGU.



HAKUSEMA MSIWE NI
MIUNGU **MINGINE** ILA
YEHOVA? SANAMU AMBAYO
MNATENGEZA KWA MIKONO
YENU INAWEZA KUWA MUNGU?

MUSA ALIIVUNJA SANAMU ILE
NA KUIFINYA HADI IKAWA LINGA.

KUTOKA 20:3-4, 32:15-20




IWAPO
UKO UPANDE WA YEHOVA BASI
KUJA HUKU USIMAME NAMI. IWAPO
LITAABUDU MIUNGU YA MISRI BASI
KAAENI MLIKO.

NI HERI
NIMFLUATE MUNGU
AWEZAYE KUGAWANYISHA
BAHARI YA SHAMU HATA
KAMA HANA PICHA.

TUTAMFLUATA
MUNGU WA
IBRAHIMU, ISAKA
NA YAKOBO.



MSHAHARA WA DHAMBI
NI MAUTI. **YHOVA** ASEMA NI
LAZIMA WAFE. BASI CHUKUENI PANGA
ZENU NA MUWAANGAMIZE WALE
WANA OABUDU SANAMU.



WATENDA DHAMBI
3,000 WALIUAWA
SIKU HIYO.

KSSHHH!


LAAA!

HURLUMIA!


KUTOKA 32:26-28

MUSA ALIKWENDA
TENA MLIMANI NA
KWA MARA NYINGINE
MUNGU ALIANDIKA
AMRI ZAKE KATIKA
MAWE MAWILI NA
KUMKABIDHI MUSA.
MUSA ALIPOREJEA
ALIWAONYESHA WATU
AMRI NA WAKAKUBALI
KUZIFUATA.






MUNGU ANASEMA NYINYI
NI WATU WENYE ROHO NGUMU.
MLIPOTENDA DHAMBI ALISEMA
MTAKUFA NYOTE ILA NILIWAOMBEA
NYOTE NA ATASAHAU DHAMBI ZENU.
KWA KWELI YEHOVA NI MWENYE
HURUMA NA MSAMAHA.



MUNGU AMEPEANA MWELEKEO WA KUJENGA
MASKANI. TUKILIJENGA KULINGANA NA ANAVYOTAKA, ATAPATANA
NASI HUKO. KWA KUWA SOTE NI WATENDA DHAMBI, MUNGU
AMETENGENEZA NJIA AMBAYO TUNaweza KUMFIKIA.

WANA WA LEVI WATATOA SADAKA
YA DAMU KILA SIKU. MARA MOJA KILA MWAKA
DAMU ITAPAKWA KWENYE SADUKU LA AGANO. MUNGU
ATAKAPOONA DAMU HIYO ATAFUTILIA DHAMBI ZETU, NA
HATUTAKUFA. NI NJIA YA MUNGU YA MSAMAHA.



NA KWA HIVYO HEKALU LILIJENGWA
KAMA WALIVYO AMURIWA
NA KILA KITU KILITENDEKA
KAMA WALIVYOAMBIWA.

LAKINI WATU
HAWAKUFURAHISHWA NA
KUISHI KWA NYIKANI HIVYO
WALILALAMIKA KILA WAKATI.

ILIKUJA SIKU AMBAYO MALALAMIKA
YAO ILIMFANYA MUNGU KUWAADHIBU.

A comic book illustration of a camp at night. Several tents are set up on a sandy ground. In the foreground, two large snakes are coiled on the ground, their heads raised. One snake on the left is looking towards the center, while the one on the right is looking towards the right. In the background, several people are gathered around a tent. One person is standing and pointing towards the right, while others are sitting or standing nearby. The sky is dark with some stars visible. A speech bubble is positioned in the upper left quadrant, containing the text 'EEEK! TAZAMENI, NYOKA WENGI.'

**EEEK!
TAZAMENI, NYOKA
WENGI.**

MUNGU ALIWATAYARISHA NYOKA WENGI WENYE SUMU KUWALIMA WATU. MUNGU NI MWNEYE HURUMA ILA HATAKUBALI WATU WATENDE DHAMBI MILELE.

KUTOKA 34:28-32, 39:32, NAMBARI 21:5-6



KAMBI LILIKUA LIMEJAA
NYOKA WENYE SUMU.



**MUNGU
TUSAIDIE!**

NYOKA WALIWAPATA HADI KWA HEMA
ZAO USIKU WALIPOKUA WAMELALA.

HISSESSSS





NISAIDIE.
NIMEUMWA.



LAAAA!

LA, JOABU!

MAMA!



**HATA WATOTO WALITESEKA KWA
DHAMBI ZA WAZAZI WAO.**

HESABU 21: 6




KILA MAHALI KWEYE KAMBI VILIO
VYA WATU VILISIKIKA. GADHABU
YA DHAMBI NI KUBWA.

KILA MAHALI
KAMBINI KUKO HIVI. TAYARI
WENGI WAMEKUFA.


LAZIMA
TUMTAFUTE MUSA.
KWA KWELI HII NI KAZI YA
MUNGU. AMEKASIRISHWA
NA DHAMBI
WANAZOTENDA WATU.

WHAACK!



LAZIMA
LUUNGUMZE NA
MUNGU. **TUNASTAHILI**
GADHABU HII ILA MSIHI
ATUHURUMIE.

WATU WATAJUA LINI
KUWA MUNGU HAPENDI
DHAMBI? LAZIMA WATII
AMRI ZAKE NA WAKUWE
TAIFA TAKATIFU.

A man with curly hair, wearing a brown robe, is shown in a deep bow of prayer. His head is touching the ground, and his hands are clasped in front of him. The background is a light blue sky with diagonal lines, suggesting a bright, open environment.

EH MUNGU. TAFDHALI
WAHURUMIE WATU WAKO NA
LIWASAMEHE DHAMBI ZAO.

**NENDA. TENGENEZA
JOKA LA SHABA KAMA ZILE
ZINAZOWALIMA WATU KISHA LIWEKE
KATIKA KIKINGI ILI WATU WAONE.
WAAMBIE WATAZAME NYOKA YA
SHABA NA WATAPONA.**

MUNGU AMETENGENEZA
NJIA. TAZAMENI NYOKA YA
SHABA NANYI MTAPONYWA.





ATAKUFA.

**LA! MUNGU
AMETENGENEZA NJIA.
FUNGUA MACHO YAKO
NA LITAZAME. TAZAMA
NA LIISHI!**



**NI
MULIJIZA!**

**LAZIMA
TUWAELEZE
WENGINE.**

**IMEFANYA
KAZI KWANGU
HIVYO ITAFANYA KWA
WENGINE.**



**TAZAMA NA
LIISHI.**

HESABU 21: 9



MBONA UNAMTANIA
NA TUMAINI LA UONGO?

WENGINE
WAMETAZAMA NA
WAMEKUWA WAZIMA.

HUONI MIMI NAAGA?
MBONA UNANISUMBLIA NA
LIJINGA KAMA HUO?



AMEKLIFA.


POLE
HAKUAMINI.

ALIKUWA
NA KIBURI
SANA.

KWA MARA NYINGINE WATU
WALILIONA UWEZO WA MUNGU. KAMBI
LILIONDOKA KWENYE MAJOKA NA
MAISHA YAKARUDI KAMA KAWAIDA.




LAKINI WATU
WALIENDELEA KUFUATA
NJIA ZAO, NA KUKOSA
KUFUATA AMRI ZA MUNGU.



WANA WA ISAEI WALILIFUATA
WINGU MUNGU ALI WALISHA KWA
CHAKULA KUTOKA MBINGUNI NA
KUWAPATIA MAJI YA KUNYWA.

ANGEWAONGOZA HADI KWENYE NCHI
ILIYOAHIDIWA ILA WALIMUASI MUNGU NA
HAWAKUFUATA AMRI ZAKE, KWA HIVYO ALIWAFANYA
WAZURURE NYIKANI KWA MIAKA 40.

MUSA, UNAFIKIRI NI WEWE TU ULIYE KARIBU NA MUNGU? SISI PIA NI WATAKATIFU KAMA WEWE NA MUNGU ANAISHI KATI YETU. HATUKUHITAJI WALA HARUNI KUTUAMURU. TUNaweza KUWAAMURU NYINYI PIA.



NDIO, NIMECHOKA KUZURURA HUKU KOTE NYIKANI NA MUNGU KUTUUA KWA SABABU NDOGO NDOGO.

NDIO, HAYA NI MAKOSA YA MUSA.

MUSA ALIKWENDA KWENYE
MASKANI NA KUMUULIZA
MUNGU ALILOHITAJI KUFANYA.





MUNGU AMEZUNGUMZA, "MNACHUKUA JUKUMA *JUU YENYU NYINYI* WANA WA LEVI. MNAWAFANYA WATU MAKUHANI KABLA YA MUNGU KUWACHAGUA."

KESHO MUNGU ATATOA HUKUMU NA TUTAWEZA KUBAINI NANI KUHANI KATI YETU. MJE HEKALUNI KESHO ASUBUHI.

NAMBARI
16:2-6



SIKU ILIYOFUATA.

KARIBIENI, NYINYI
MNAOTANGAZA UTAKATIFU WENU,
NYINYI AMBAO MNGEKUWA MAKUHANI
NA KUWAONGOZA WENZENU.

MUNGU ATAKUTANA NASI LEO
HAPA NAYE ATACHAGUA. TUTAONA
NGUVU ZAKE NA UTUKUFU.




**JITENGENI NA WATU
HAWA WAOVU KWA DAKIKA
MOJA NITAWAANGAMIZA.**



**ONDOKENI KATIKA
HEMA ZAO. MSIWAKARIBIE
AMA NYINYI PIA MTAKLIFA
NAO.**





HAPA KUNA JARIBIO: WATU
HAWA WAKIFA KIFO CHA KAWAIDA
MTAJUA MIMI NI NABII WA UONGO NA
MUNGU HAZUNGUMZI NAMI.

LAKINI IWAPO LEO
MTAONA JAMBO JIPYA
LIKITENDEKA, DUNIA IKIFUNGUKA
NA IWAMEZE PAMOJA NA
VITU VYAO HADI JEHANAMU,
MTAFAHAMU KUWA WALITENDA
DHAMBI DHIDI YA MUNGU NA
KUWA MIMI NI NABII WAKE.



SAIDIA!


YIEEE!

LAAAA!

HESABU 16:28-33




WATU WOTE WALIOJIFANYA MAKUHANANI
WALIMEZWA MZIMA MZIMA HADI
KWENYE MOTO WA JEHANAMU.



CHUKLIA
VYOMBO VYAO VYA
SHABA NA UVITUMIE
KUTENGENEZA KIFUNIKO
CHA MADHABAHU.

MTAKAPO ONA SHABA IKIFUNIKA
MADHABAHU MTAKUMBUKA SIKU HII, AMBAYO
WATU WALIASI AMRI ZA MUNGU NA WAKATAKA
KUJIFANYA MAKUHANI WENYEWE.


HIO ILIKUA NI SIKU
AMBAYO WANA
WA ISARAELI
HAWANGEWAI
SAHALI. MUNGU
ALIDHIBITISHA KUWA
MUSA ALIKUWA
NABII WAKE, NA
WALE TU AMBAO
ANGEWACHAGUA
NDIO WANGEKUWA
MAKUHANI WAKE.



UTUKUFU WA MUNGU
LIPO NASI NAYE
HUTUPATIA MKATE
KUTOKA MBINGUNI.

UTUKUFU WA MUNGU SIKU ZOTE ULISIMAMA
JUU YA MASKANI NA WATU WALIMFUATA MUSA
NYIKANI KWA MIAKA 40 KWA HIARI YAO.


MUNGU ALIENDELEA KULETA MKATE
TOKA JUU MBINGUNI, NA ALIWAPA MAJI
KUTOKA KWA MWAMBA. ILE NGUZO YA
MOTO ILIWAFUNIKA USIKU NA WINGU
MCHANA. WAKATULIA NA WAKAJIFUNZA
KUFUATA AMRI ZA MUNGU.



MAKUHANI WALISHUGHULIKIA
HEKALU NA WALITOA SADAKA KILA
SIKU KAMA MUSA ALIVYOAMURU.



BAADA YA MIAKA 40 NYIKANI, KILA MTU ALIPOKUWA AKIJITAYARISHA KUINGIA KWENYE ARDHI ILIYOAHIDIWA, MUNGU ALIMUITA MUSA MLIMANI. HUKO BAADA YA KUZUNGUMZA NA MUNGU KWA MARA YA MWISHO, ALILALA CHINI KWA LIPOLE NA KUAGA DUNIA.



GHAFLA, ROHO YAKE ILIELEKEZWA
KWENYE UWEPWA WA MUNGU. HAPU,
ANGEKAA HADI MWISHO WA NYAKATI
AMBAPO ANGEUNGANIKA TENA NA
WATU WAKE KWENYE NCHI AMBAYO
MUNGU ALIAHIDI IBRAHIMU.

TAKRIBAN MIAKA 1451 KABLA YA KRISTO - KUMBUKUMBU LA TORATI 34:4-5

KARIBU MIAKA 500 ILIPITA BAADA
YA IBRAHIMU KUELEZWA NA MUNGU
AWACHE WATU WAKE NA KUENDA
AMBAKO MUNGU ANGEMUELEKEZA.




AHADI YA MUNGU KWA IBRAHIMU NA
SARA YA KUWAPA TAIFA KUBWA KUPITIA
KWA MWANAO ISAKA ILITIMIA. WATOTO
12 WA YAKOBO, AMBAYE JINA LAKE
LILIBADILISHWA NA KUWA ISRAELI,
WALIKUWA NI KABILA 12 YA WATU.





WALITOKA UTUMWANI, WAKAZURLUZA
JANGWANI, WAKAPOKEA
AMRI ZA MUNGU NA SASA
HATIMAYE WALIKUWA WANAINGIA
KWENYE NCHI WALILOAHIDIWA.
WALIPOKUWA NYIKANI KULIKUWA
NA KIJANA MMOJA MDOGO
AMBAYE ALITEMBEA KANDO YA
MUSA AKIJUFUNZA JINSI YA
KUONGOZA TAIFA LA ISRAELI.




KIJANA HUYO
ALIKUWA MKUBWA NA
ALIITWA YOSHUA.

BAADA YA MUSA KUFUFA, YOSHUA
ALICHAGULIWA NA MUNGU ILI KUONGOZA
WATU KWENYE NCHI ILIYOAHIDIWA IBRAHIMU.



WATU WALIKUMBUKA UNABII KWAMBA WANGEKUWA
WATUMWA KATIKA NCHI YA LIGENI NA KWAMBA
BAADA YA MIAKA 400 WANGERUDI KWENYE CHI
YA BABA ZAO. MUNGU ALITIMIZA HUO UNABII.



SIKU HIYO WALIVUKA
MTO YORODANI,
CHAKULA TOKA
MBINGUNI KIKAISHA
NA WAKALA CHAKULA
KUTOKA KWENYE
NCHI HIYO.

EEEE MUME
WANGU. HUKU NI
KUZURI AMBAKO MUNGU
AMETULETA SISI.

KUMBUKUMBU LA TORATI
34:9, YOSHUA 5:12

NDIO. NI MAHALI PAZURI PA
KIWALELEA WATOTO WETU KWA
UNYENYEKEVU NA AMANI.



<https://goodandevilbook.com/>